SOMO LA 24

MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU YESU KAMA MFALME WA ULIMWENGU

"Na tazama, utachukua mimba katika tumbo lako, na kuzaa mtoto mwanamume na jina lake utamwita Yesu, Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu ATAMPA KITI CHA ENZI CHA BABA YAKE DAUDI, na hivyo ataitawala nyumba ya Yakobo milele, na ufalme wake hautakuwa na mwisho "- Luka 1: 31,33.

"Na awe na enzi toka bahari hata bahari, Toka Mto hata miisho ya dunia .... Naam, wafalme wote wataanguka chini mbele yake: mataifa yote watamtumikia yeye" - Zaburi 72:8,11.

Dondoo hili linaunganisha kwa ufanisi mafundisho ya maandiko matakatifu ya UTAWALA wa Yesu Kristo kwa ahadi alizopewa Ibrahimu na Daudi. (Kama ni muhimu, pitia masomo 22 & 23 ya: Ibrahimu na Daudi)

Biblia inafundisha wazi kwamba wakati unakuja ambapo Mwana wa Mungu, aliye sasa mbinguni, ataonekana wazi atakaporudi duniani, kuondolea mbali serikali zote za wanadamu na madaraka yao, na ajiimarishe badala yao kama mtawala wa wanadamu wote. Somo la 21 liligusia juu ya somo hili, na madhumuni ya somo hili yatakuwa kuingia kwa undani zaidi na kuonyesha jinsi kipengele maarufu zaidi cha tabia ya Yesu Kristo, kama ilivyoelezwa kwenye Maandiko yote, ni UTAWALA wake.

Ufalme wa Kristo ni mada isiyotiliwa maanani na Ukristo wa jadi. Hutolewa kwa "kinywa", lakini nadharia ya mbinguni kama mahali pa kuu pa zawadi inaharibu na kuondoa umuhimu wa kumtambua Kristo kama Mfalme wa ulimwengu. Kama mtu anasema, Yesu ni Kristo, au mpakwa mafuta, wakati akiwa na wazo la kimakosa kabisa basi maneno hayo ni sauti tupu. Utambuzi wa jadi wa ufalme wa Kristo kwa ujumla unaeleweka kuwa zoezi la sasa ambalo ni mamlaka yake Kristo ya kiroho mbinguni. Hili linapuuza maoni yaliyowasilishwa katika maandiko.

Matarajio ya Wayahudi kwa Masihi yalikuwa ni kwamba anafaa kuonekana nchini, na awe na nguvu za kifalme juu ya mataifa yote. Wanafunzi wa Yesu wenyewe walikuwa na mtazamo huo. Utata halisi ni kama mtazamo huu ni sahihi. Kwa ujumla, Theolojia ya jadi hupuuzilia mbali mtazamo huu kuwa ni kosa kuu la mawazo ya kimwili ya kibinadamu, na inakashifu wazo la ufalme hapa duniani kinyume hasa na mtazamo wa Ukristo.

Je, Biblia inatufunza nini? Matarajio yaliokuwa ya wanafunzi ni ya makosa na ya kidunia? Kama ni hivyo, basi tunakabiliwa na matatizo makubwa.

Kwanza, Kristo mwenyewe hakusema mtazamo wa wanafunzi wake kuhusu Masihi na ufalme wake ulikuwa ni wa makosa na wa kimwili.

Pili, wakati baadhi ya wanafunzi hawa baadaye walipoandika nyaraka ambazo sasa ni sehemu ya Agano Jipya, imani hii haikubatilishwa wala kuwa tofauti na hizo zilizonekana humo. Kwa kweli, ushahidi wote wa maandiko unaunga mkono mafundisho haya ambayo ni jambo la kawaida kuyahukumu au kuyakataa.

Yesu akawaambia wale waliomsikiliza, "sikuja kuharibu sheria na manabii, bali kutimiza" - Mathayo 5:17.

Hakuna taarifa inayoweza kuwa ya wazi zaidi kwa kazi ya Kristo. Lakini nini, hasa, ndicho manabii walisema kumhusu yeye?

MTAZAMO WA UNABII WA UTAWALA WA KRISTO

"Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa MTAWALA KATIKA ISRAELI." - Mika 5:2. Nani alitoka Bethlehemu? Yesu wa Nazareti. Hili ni la msingi wa kinabii kuhusu kumtambua yeye kama "mtawala katika Israeli" wa baadaye. Mada hii inaungwa mkono na maneno ya Yeremia ... "Tazama, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapomchipushia Daudi Chipukizi la haki; naye atamiliki mfalme, atatenda kwa hekima, NAYE ATAFANYA HUKUMU NA HAKI KATIKA NCHI: katika siku zake Yuda ataokolewa, na Israeli atakaa salama "- Yeremia 23:5,6.

Je, nini inaweza kuwahamasisha Wayahudi na kuwapa matumaini ya kitaifa ya kuwa na mfalme halisi na ufalme halisi? Nani ndiye "tawi la haki la Daudi?" Hakuna mwingine ila Yesu maana yeye mwenyewe anadai nafasi hiyo - "Mimi ni mzawa wa ukoo (au TAWI: ‘mzao’ ikiwa kwamba ambalo hukua nje ya 'mzizi') wa Daudi ..." - Ufunuo 22:16.

Kristo akiwa Tawi la Haki aliyeteuliwa kwa Daudi, na amekuja kutimiza sheria na manabii, lazima "atawale na kufanikiwa, na kutekeleza hukumu na haki KATIKA NCHI": kwa maana nabii ametangaza Tawi la Haki atafanya hivyo. Wazo hili halitokei katika kauli moja au mbili, lakini linaonekana katika shuhuda nyingi za unabii, kama ilivyoelezwa katika vibandiko vya kando…

VIBANDIKO VYA KANDO: SHUHUDA ZA UNABII WA AGANO LA KALE KUHUSU UTAWALA WA KRISTO "Tazama, siku zinakuja, asema Bwana, ambapo nitatekeleza jambo jema nililolinena kwa nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Katika siku hizo na wakati huo, nitasababisha chipukizi la haki kukua kwa Daudi, naye atafanya hukumu na haki katika nchi hii. " - Yeremia 33:14-15. "MAANA kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume, na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake, na jina lake ataitwa, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi, na ufalme wake, kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele. wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo "- Isaya 9: 6,7. "Tazama mtu huyu ndiye ambaye jina lake ni Chipukizi; naye atakua katika mahali pake ...; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi,

naye atakuwa kuhani juu ya kiti chake" - Zekaria 6:12-13. "Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi, nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu: Taifa halitainua upanga juu ya taifa, wala hawatajifunza vita tena kamwe" - Isaya 2:4. "Naye Bwana atakuwa Mfalme juu ya nchi yote; siku hiyo kutakuwa na Bwana mmoja, na jina lake moja" – Zekaria 14:9.

"Tazama, mfalme atamiliki kwa haki, na wakuu watatawala kwa hukumu" – Isaya 32: 1. "Bwana wa majeshi atatawala katika mlima wa Sayuni, na katika Yerusalemu, na mbele ya wazee wake kwa utukufu" - Isaya 24:23. "Dunia itajawa na kumjua Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari. Na itakuwa katika siku ile shina la Yese, lisimamalo kuwa ishara kwa kabila za watu, yeye ndiye ambaye mataifa watamtafuta. Na mahali pake pa kupumzikia patakuwa na utukufu "- Isaya 11: 9-10. "Piga Kelele mwenyeji wa Sayuni; kwa kuwa Mtakatifu wa Israeli ni mkuu kati yako" - Isaya 12:6. "nami nitawafanya (Wayahudi) kuwa taifa moja katika nchi hiyo, juu ya milima ya Israeli, na mfalme mmoja atakuwa Mfalme wao wote" - Ezekiel 37:22. "Bwana amemwapia Daudi neno la kweli hatarudi nyuma akalihalifu, Baadhi ya wazao wa mwili wako Nitawaweka katika kiti chako cha enzi" - Zaburi 132: 11. "Neno la BWANA kwa Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume mpaka nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako. Bwana atainyosha toka Sayuni Fimbo ya nguvu zako. Uwe na enzi kati ya adui zako.." - Zaburi 110:1, 2. " Uniombe nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako" - Zaburi 2: 8. "Na awe na enzi toka bahari hata bahari, Toka Mto hata miisho ya dunia .... Naam, wafalme wote wamsujudie; mataifa yote watamtumikia yeye" - Zaburi 72: 8.11. (Angalia pia Dan 7:14). (MWISHO WA vibandiko vya kando).

Hii ni baadhi tu ya taarifa nyingi ambazo Biblia husema kuhusu somo hili. Ni wazi, matarajio ya Wayahudi na wafuasi wao yalikuwa sawa. Manabii walionyesha wazi wazo hili moja la kurudi kwa Kristo duniani kama mfalme; na kama Wayahudi hawakuwa sahihi katika kutazamia dhihirisho hilo, haikuwa makosa yao. Sio kwa sababu walikuwa na nia ya kimwili; lakini kwa sababu lugha ya watu watakatifu waliowatangulia, waliosema kama walivyoongozwa na Roho Takatifu, waliwaandaa kutupilia mbali dhana yoyote ile, isipokuwa wazo moja hilo la ufalme duniani.

KUUNGA MKONO AGANO JIPYA

Lakini Agano Jipya nayo je? Je, linatupa mwanga mwingine juu ya kauli ya Agano la Kale, na hivyo kudhoofisha kuungwa mkono kwa mafundisho ya Wayahudi kuhusu ufalme wa Masihi? Ni kawaida kudhania kwamba ndivyo ilivyo, lakini kutokana na uchunguzi usioegemea upande wowote yaonekana kuthibitisha kuwa Agano Jipya bila shaka linaambatana na mafundisho ya manabii juu ya somo hili. Hapo awali kuna ujumbe uliotolewa na malaika Gabrieli kwa Mariamu, katika kutangaza kuzaliwa kwa Kristo: "Na tazama, utachukua mimba katika tumbo lako, na kuzaa mtoto mwanamume na utamwita jina lake Yesu, Yeye atakuwa. mkubwa, na ataitwa Mwana wa Mungu mkuu. Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Baba

yake DAUDI, na hivyo ataitawala nyumba ya Yakobo milele, na ufalme wake hautakuwa na mwisho " - Luka 1:31,33.

Hapa ni tamko bayana la Agano Jipya kwamba ni lengo la Mungu kumpa Yesu "kiti cha enzi cha Daudi baba yake." Tumeona Daudi na ahadi za Mungu kwake katika Somo la 23. Tunajua kwamba Daudi alikuwa mashuhuri zaidi ya wafalme wa Mungu waliotiwa mafuta Israeli, akitawala juu ya makabila kumi na mawili ya Israeli katika Nchi Takatifu, na kutawala mataifa mengi ya kando. Alikuwa shujaa mwenye nguvu, nabii anayejulikana, na mshairi mahiri wa aina ya kipekee. Daudi alikuwa baba wa Kristo, kwa njia ya Mariamu, ambaye alikuwa wa ukoo wa nyumba ya kifalme. Lakini nini maana ya "KITI CHA ENZI CHA DAUDI"?

Petro alisema, katika hotuba yake kwa Wayahudi katika siku ya Pentekoste: "Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake (Daudi) kwa jinsi ya mwili, yeye atamuinua Kristo KUKETI KWENYE KITI CHAKE CHA ENZI."- Matendo 2:30.

Kwa hivyo, kuna uhusiano kati ya ujumbe wa Kristo na kiti cha Daudi. Je, Daudi alikuwa na kiti cha enzi? Alikuwa nacho. Kilikuwa na nini? Ni wazi kuwa kiti cha juu ambacho alikalia kwa muda mrefu kimevunjika na kuwa vumbi. Kiti cha enzi cha ufalme ni zaidi ya kiti halisi kilichorembeshwa kinachomilikiwa na mkubwa katika hafla ya serikali. Tunaposema kuhusu kiti cha enzi cha Uingereza, tunamaanisha afisi, kazi au nafasi ya Mfalme nchini humo. Kadhalika kwa kiti cha enzi cha Daudi. Mtazamo maarufu wa makanisa ni kwamba Kristo sasa yuko kwenye kiti cha Daudi. Lakini wapi ambapo ni eneo la utawala wa sasa wa Kristo? Kristo yuko mbinguni, anakaa na Baba yake katika kiti cha enzi cha Baba yake, lakini si kwenye kiti cha Daudi. Hakuna kitu ambacho Daudi alimiliki ambacho kiko mbinguni, kwa hivyo haiwezekani kuwa Kristo sasa ameketi juu ya kiti hicho cha enzi. Daudi mwenyewe hayuko mbinguni; kwa kuwa Petro alisema katika hotuba yake ya siku ya Pentekoste ... "Daudi hakupanda mbinguni." - Matendo 2:34

Biblia inafundisha kuwa wakati ujao ulioteuliwa na Mungu, kiti cha Daudi kitarejeshwa tena katika ardhi na Yesu atakishirikisha waaminifu wake ... "Katika siku hiyo nitainua tena maskani ya Daudi iliyoanguka" - Amosi 9.11. "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi." - Ufunuo 3:21.

Yesu alisema kuhusu huo wakati alipokuwa duniani. Alisema ... "Atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atapoketi katika kiti cha utukufu wake." - Mathayo 25:31

Kwa hiyo, kabla ya Yesu kukaa juu ya kiti cha enzi cha Daudi, atarudi duniani, aonekane Palestina, na kuchukua nafasi ambayo Daudi alimiliki wakati alipokuwa mwenye Fimbo ya utawala wa Israeli; yaani, atakuwa mfalme wa Wayahudi.

Ili kuelewa kikamilifu tangazo la malaika kwa Mariamu, ni muhimu kutambua kwamba ni lazima kuhusishwa katika mazingira ya unabii wa Mungu yaliyotamkwa na kuandikwa na Ezekieli miaka zaidi ya 600 iliyopita. Nabii alitumwa kwa Mfalme wa mwisho kuchukua kiti cha Daudi - Mfalme Sedekia. Alikuwa mkuu asiyestahili, na Ezekieli alitumwa kumwambia juu ya adhabu iliyotarajiwa kumpata. Katika mfululizo wa unabii wake, alisema maneno yafuatayo: "Na wewe, Ewe mtu mwovu, uliyetiwa jeraha kiasi cha kuua, mkuu wa Israeli, ambaye siku yako imekuja, katika wakati wa uovu wa mwisho, Bwana MUNGU asema hivi: Kiondoe kilemba, ivue taji; haya hayatakuwa tena kama yalivyo; kikweze kilicho chini, kakishushe kilichoinuka. Nitakipindua, nitakipindua nitakipindua; hiki nacho hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake, nami nitampa" - Ezekiel 21: 25-27. Hili lilikuwa tamko kutangaza mwisho wa ufalme wa Mungu kama ulivyokuwepo hapo nyuma. Kilemba kilifaa kiondolewe, kisha taji ivuliwe, na taifa la kisiasa linalojulikana kama Ufalme wa Israeli kuondolewa kabisa, kama ilivyoainishwa katika marudio ya mara tatu ya kitenzi, "kipindue)," na kama ilivyoonyeshwa kwa maneno, "hayatakuwa tena."

Utabiri unaohusiana na mambo ya Wayahudi, hata mambo ambayo huwa ya enzi ya Daudi, na utimilifu wake ni wa sifa mbaya kwa kila msomaji wa historia ya Wayahudi. Mwaka mmoja baada ya utabiri huu kufanyika, ya kwanza kwa vamizi tatu (zinazotokea Kabla Kristo(BC) 606, 598 & 587 kwa mtiririko huo) kwa Wababeli chini ya Mfalme Nebukadneza kutokea. Matokeo yalikuwa janga kubwa na machafuko kwa taifa la Israeli.

Sedekia hakuwa ametuzwa, watu wenye cheo waliuawa, taifa hilo kwa kiasi fulani kilifanyiwa unyama, na sehemu kiasi kilichukuliwa mateka, na ardhi ikawa na uharibifu mkubwa. Miaka sabini baadaye, marejesho sehemu fulani ulifanyika chini ya Ezra na Nehemia, lakini si ya kiti cha enzi cha Daudi. Wayahudi walikuwepo kama vibaraka kuanzia hapo; na baada ya tawala mbalimbali za kisiasa, walivamiwa na dhoruba la Kirumi katika mwaka wa 70 (Baada ya kuzaliwa Mwokozzi) ambayo iliyotupilia mbali kila sehemu ya maisha yao ya kitaifa.

Lakini hii hali ya kiti cha Daudi inafaa kubaki hivi daima? Unabii uko wazi kabisa: hali ya ukiwa itaendelea "hadi atakapokuja yeye ambaye ni haki yake." "YEYE" ni nani? Si mwingine ila MMOJA aliye katika unabii wa Agano la Kale - yaani, Yesu Kristo, ambaye kiti cha enzi kinafanywa kiwe haki yake, kulingana na ukoo, na mrithi wa kipekee upande wa Mungu. Angalia kwa makini kuwa ni vitu vilivyopinduliwa (kilemba, taji, kiti cha enzi, na Ufalme wa Daudi) ambavyo ni vitu vya kupewa Kristo wakati atakapokuja. Kwa wakati huo atakuwa Mfalme wa Wayahudi, na Bwana wa dunia yote. Katika muktadha huu na umuhimu wa kushangaza kwa maneno ya malaika: "Bwana Mungu atampa, YESU KITI CHA ENZI CHA BABA YAKE DAUDI, na hivyo atautawala UKOO WA YAKOBO milele, na UFALME WAKE hautakuwa na mwisho."

Kwenda hatua zaidi katika uchunguzi wetu wa Agano Jipya, tunakuja kwa kuzaliwa kwa Kristo, na tunaona tukio hili: "Basi wakati Yesu alizaliwa mjini Bethlehemu, mkoani Yudea, wakati

Herode alipokuwa mfalme, Basi, wakaja watu wenye busara kutoka mashariki ya Yerusalemu, wakisema, wapi yeye aliyezaliwa MFALME WA WAYAHUDI "- Mathayo 2:1.

Bila shaka watu wenye busara walielewa umuhimu wa tukio hili katika mazingira sawa ya manabii wote walivyokuwa wametabiri juu yake huyo wa kutawala katika Israeli. Wao walielewa kwamba atakuwa MFALME WA WAYAHUDI. Mafundisho ya jadi ya mkutano wa Ukristo ni kwamba Kristo ni mwokozi wa kiroho wa wanadamu, kwa maana ya jumla ya uhusiano mpana wa kiroho kwa binadamu kwa ujumla; na kwamba yeye ni mfalme wa wale ambao huleta wokovu – Wayahudi wa kiroho, ambao sio Wayahudi nje haswa, lakini ndani ya moyo. Lakini Kristo hajawahi kudai kuwa mfalme wa kondoo wake wa kiroho. Kwa wao, husema, "Mimi siwaiti tena watumwa, lakini marafiki." Wao ni ndugu zake, "warithio pamoja na Kristo" (Warumi 8:17), nao watatawala pamoja naye kwa miaka elfu moja (Ufunuo 20:6). Wao sio wake, lakini kwa kiasi kikubwa bibi yake, "mke wa Mwana-Kondoo" - likimaanisha ushirika wa karibu na utambulisho wa maslahi ya kimahusiano. Kristo, kwa hiyo, hawezi kuwa mfalme wa Wayahudi katika maana yoyote ya kiroho. Yeye ni mfalme wa Wayahudi hao ambao Daudi alikuwa mfalme; kwa maana ni mrithi wa kiti chake. Kwamba hii ilikuwa asili ya madai yake, kama inavyoeleweka na watu wa siku zake, ni dhahiri kutokana na yale ambayo mfalme Herode alijibu, "Mfalme Herode aliposikia hayo alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye. Mara baada ya kuwakusanya pamoja makuhani wakuu wote na walimu wa Sheria pamoja, akawauliza mahali ambapo Kristo atazaliwa. Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi. ndivyo nabii alivyoandika, na Ewe Bethlehemu katika nchi ya Yuda, hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; maana kwako atakuja Gavana, atakayetawala watu wangu Israeli na (Herode) akatuma watu akawaua watoto wote wa kiume mjini Bethlehemu...na katika pwani yake wenye umri wa miaka miwili na chini, kulingana na muda aliopata kujua kutoka kwa wale wenye hekima "- Mathayo 2: 2,3,6,16. Ni dhahiri kwamba Herode alielewa tangazo hili kama tishio moja kwa moja na changamoto kwa afisi yake na nafasi kama mfalme - ingawa nafasi hiyo ilikuwa ndogo zaidi kama kuisimamia koloni ya Kirumi kama "Mfalme wa Wayahudi" kwa jina la Kirumi Kaisari. Ingekuwa ya umuhimu kidogo kwa Herode kama Kristo angekuwa tu mtawala wa kiroho akitawala kwa nguvu zake akiwa mbinguni katika mioyo ya watu. Hiyo kwa njia yoyote haingekuwa na mgogoro na utawala wa Herode kuwa mfalme. Hata hivyo, majibu yake ya unyama yanatumika kama ushahidi kwamba alimtambua Kristo kama mdai mtarajiwa wa ufalme halisi wa Israeli.

Kama tunafuatilia kazi na tunakumbuka maneno ya Kristo, kama ilivyorekodiwa zaidi, tutapata dalili mara kwa mara ya usahihi wa maoni yanayokaribishwa na mitume kuhusu utawala wake. Kwa mfano, katika kipindi cha mahubiri yake mlimani, alisema: "Usiape kwa Yerusalemu, maana ni mji wa Mfalme mkuu." - Mathayo 5:35.

Hapa Kristo anafanya uhusiano kati yake na mji ambao ulishuhudia fedheha yake, na anachukulia muunganisho kuwa takatifu kwamba haruhusu> kutumia jina la mji kwa kiapo. Yeye ni "Mfalme mkuu". - "mkubwa kuliko Sulemani." Yerusalemu ni mji. Ulikuwepo wakati huo Kristo akitamka maneno haya tunayoyazingatia. Wakati huo ulikuwa ni mji wenye

mafanikio makubwa, na penye mrahaba na kisoma. Punde, katika mwaka wa 70 (Baada Kifo cha Kristo), ulitekwa nyara na hadhi yake ikashushwa na Warumi, na imebakia katika ukiwa hadi nyakati za hivi karibuni. Hii ilitabiriwa na Bwana Yesu. Alisema: "Wao (Wayahudi) watauawa kwa upanga, wengine watachukuliwa mateka katika nchi zote, na Yerusalemu utakanyagwa na watu wa mataifa mengine, hadi nyakati zao zitakapotimia" - Luka 21:24.

Pia alisema (kwa huzuni mkubwa): "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, Unawaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwako! Mara ngapi nimetaka kuwakusanya watoto wako pamoja hata kama kuku anavyokusanya vifaranga vyake chini ya mbawa zake, lakini hukutaka. Tazama, nyumba yenu imeachwa tupu na ukiwa. Kwa maana nawaambia, ninyi hamnioni tena mpaka siku ile mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana "- Mathayo 23:37-39; Luka 13:34,35

Hapa kuna utabiri wa kukanyagwa na kufanywa ukiwa. Utabiri huu wa Kristo ni sambamba na unabii wa Ezekiel ulioangaziwa katika ukurasa wa 3. Kumbuka kuwa kuna mpaka unaotokana na kuharibiwa kwa Yerusalemu, na mpaka huo unatupa ratiba ambayo inapima kiwango cha utawala wa watu wa Mataifa wa kidunia. Kwa mujibu wa utabiri huu, Yerusalemu itapata nafuu kutokana na kuanguka kwake wakati wa kufika kwa kipindi kilichoandikwa kwa neno "hadi". Kristo alisema kuwa matukio mawili yatatambulisha wakati huo: 1) nyakati za kukamilika kwa Mataifa na, 2) taifa la Wayahudi kutambua msulubishwa Yesu kama anayebeba jina la Mungu. Matukio yote ni ya hakika, na sisi tunapewa taarifa, katika ushahidi ufuatao, kwamba siku inakuja ambapo Kristo atapokelewa na watu wake waliotubu-Wayahudi: "Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma, nao watamwombolezea kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake kama mmoja aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wa kwanza wake " - Zekaria 12:10 Wakati hayo yametendeka, nini basi kitafanyika Yerusalemu? Kwa mara nyingine, Agano la Kale linatoa ushuhuda wa kinabii unaotoa jibu kushawishi (tazama vibandiko vya kando)

VIBANDIKO VYA KANDO: UNABII WA AGANO LA KALE KUHUSU HATIMA YA YERUSALEMU "Bwana atairithi Yuda, iwe sehemu yake katika nchi takatifu, naye atachagua Yerusalemu tena" –Zekaria 2:12 "Bwana atafariji Sayuni; Yeye atafariji maeneo ya taka yake yote na jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni, na nyika yake kama bustani ya Bwana; furaha na kicheko zitaonekana ndani yake, kushukuru, na sauti iliyo nzuri"- Isaya 51:3

" Amka, amka, jivike nguvu zako, Ee Yerusalemu, Wewe uliyenywea, mkononi mwa Bwana, kikombe cha hasira yako: Bakuli la kikombe cha kulevya-levya Umelinywea na kulimaliza ... .. Basi, kwa sababu ya hayo, ulisikilize neno hili,ewe uliyeteswa, na kulewa, lakini si kwa mvinyo, BWANA, Bwana wako , na Mungu wako awateteaye watu wake asema hivi, Tazama nimeondoa mkononi mwako kikombe cha kulevya-levya, hilo bakuli la kikombe cha hasira yangu; hutakinywea tena; "- Isaya 51:17,21,22 "Amka, amka, jivike nguvu zako, Ee Sayuni; jivike mavazi yako mazuri, Ee Yerusalemu, mji mtakatifu, Kwa maana tokea sasa hataingia ndani yako

Asiyetahiriwa wala aliye najisi. . . Pigeni kelele za furaha, imbeni pamoja, Enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa, kwa kuwa Bwana amewafariji watu wake, ameukomboa Yerusalemu. "- Isaya 52:1,9 “Bwana wa majeshi atatawala katika mlima wa Sayuni, na katika Yerusalemu, na kabla wazee wake kwa utukufu "- Isaya 24:23 “Wakati ule watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha BWANA na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu, kwa ajili ya jina la Bwana, kwa Yerusalemu ; wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa mioyo yao mbaya "- Yeremia 3:17" Kwa maana sheria itatoka katika Sayuni, na neno la Bwana katika Yerusalemu; naye atafanya hukumu katika watu wengi, naye atawakemea mataifa wenye nguvu walio mbali; nao watafua panga zao ziwe majembe na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa, wala hawatajifunza vita tena kamwe "- Mika 4:2,3 (MWISHO WA vibandiko vya kando)

Hivyo tunatambua kuwa mji wa Yerusalemu una nafasi muhimu katika kusudi la Mungu. Ina elekea kuwa mahali pa serikali ya Mungu ambayo itabariki dunia nzima katika siku za usoni utakuwa, kwa kweli, mji mkuu wa ufalme wote unaokuja, pakiwa ni kituo cha nguvu, cha sheria, ya kutamalaki, kwani mataifa yatathamini. tena watatembelea huko kwa ajili ya kufundishwa katika huo utukufu: "na mataifa wengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia yake, na sisi tutakwenda katika mapito yake, kwa maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalemu "- Isaya 2:3

Bwana Yesu alijua vizuri kusudi hili tukufu katika kuhifadhiwa kwa mji. wa Yerusalemu. Akiwa na hili akilini mwake, na kwa manufaa ambayo yanaweza kupatikana na kukubaliwa na wale ambao wanaelewa madhumuni ya Mungu, anaweza kusema, "Usiape kwa Yerusalemu, maana ni mji wa Mfalme mkuu." Hivyo sisi tunawezeshwa kunukuu maneno ya Kristo katika "mahubiri ya mlimani", ushahidi wa nguvu ya ukweli wa utawala wake kuhusiana na dunia.

Zaidi ya hayo, Nathanieli ("Mwisraeli kweli kweli, ambaye hakuna hila") anaongeza kwa ushahidi huu katika kumtambua kwake Kristo: "Mwalimu, wewe ni Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli" - Yohana 1:49. Kukubalika kwa haya kwaonyeshwa katika maneno ambayo yavuta hisia na mawazo ya watu kwa mafundisho ya Kristo; ni dhahiri na ukweli kwamba "walitaka kumkamata kwa nguvu, ili kumfanya mfalme" - Yohana 6:15

Lugha yao, juu ya tukio la kuingia kwake kwa ushindi katika mji wa Yerusalemu, ni ushahidi tosha juu ya jambo hili: "Heri mtu ajaye kwa jina la Bwana. Ubarikiwe ufalme ujao wa baba yetu Daudi ajaye kwa jina la Bwana!" - Marko 11:10

Hata hivyo, viongozi wa Wayahudi walipanga maangamizi yake, na walifanikiwa katika mipango yao ya fujo. Wao wakampeleka kwa Pilato, ambaye hakumpata na hatia yoyote, akawa na nia ya kumwachilia (Luka 23: 13-16). Hili liliongeza uhasama wao, na ikadhihirisha sababu za kweli kwa chuki zao kwa Yesu. Wao wakapiga kelele wakisema - "Kama wewe basi utamwachilia huyu mtu, wewe si rafiki yake Kaisari; kila mtu anayejifanya kuwa MFALME humpinga Kaisari!" - Yohana 19:12

Hili lilikuwa na athari mwafaka: Pilato akatoa hukumu; na Kristo akasulubiwa, na kulingana na desturi ya Kirumi, hali ya mashtaka juu yake yakawekwa wazi kwa maandishi juu ya ule mti, "Yesu wa Nazareti, MFALME WA WAYAHUDI" - Yohana 19: 9

Hapa tena ufalme wa Kristo ulikuwa wa mbele na katikati. Alisulubiwa kwa sababu "alijifanya mwenyewe kuwa mfalme" (Mathayo 27:11). Hili ni tamko la yale yaliyoandikwa pale. Chapisho hilo halikuwapendeza makuhani wakuu ... "ilani hiyo ilisomwa na Wayahudi wengi ..... Basi, makuhani wakuu wa wayahudi wakamwambia Pilato, usiandike, Mfalme wa Wayahudi, bali kwamba YEYE ALISEMA, mimi ni Mfalme wa Wayahudi. "- Yohana 19:20-21. Hapa ni ushahidi muhimu kutoka kwa makuhani wakuu kwa madai ya Kristo mwenyewe wa mrahaba wake. Kwa kweli maonyesho ya maisha ya Bwana wetu duniani siku za mwishomwisho labda ni ushahidi zaidi wa maamuzi kwamba mrahaba mtarajiwa wa Wayahudi ulikuwa kipengele muhimu ya tabia yake kama Masihi - kipengele ambacho huondolewa kabisa katika mahubiri maarufu. Mafundisho ya Mitume baada ya kupaa kwa Kristo yalikuwa ni haya haya. Tunasoma kwamba Wayahudi wa Thesalonika walifanya mashtaka kuwahusu wao kwa wakubwa wa mji kwa mtindo huu: "Watu hawa ambao wamepindua dunia nzima, wamefika huku pia ambapo Yasoni amewakaribisha nyumbani kwake, na hawa wote wanafanya kinyume cha amri ya Kaisari, wakisema na KWAMBA KUNA MFALME MWINGINE, AITWAYE YESU "- Matendo 17:6,7.

Paulo aliyakariri hayo kwa watu wa Athene, katika hotuba yake Mlima wa Mars ..." na wakati wa huo ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu, kwa sababu Yeye amekwisha weka siku atakayowahukumu (ambayo, kwa matumizi yake ya kisiasa, maana yake ni kutawala) ulimwengu kwa haki kwa njia ya MTU MMOJA ALIYEMTEUA, ambao amewathibitishia wote mambo haya kwa kumfufua katika wafu. " - Matendo 17: 30,31

Kwa kweli, MADA kubwa ya mafundisho ya Agano Jipya juu ya Yesu ni kuwa yeye ni "Kristo," yaani, "Mpakwa mafuta," Yeye aliyetabiriwa na manabii kama mfalme wa baadaye wa ulimwengu. Kumkatalia kwake ufalme huu ni kukataa kuwa yeye si Kristo - kwani "upako" unamaanisha, sio tu kuhusu tabia yake kama "Mwanakondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu," bali kwa maendeleo yake ya baadaye kama mteuliwa wa Mungu, MFALME duniani. Jina lake "Kristo" ni mtazamo, unaofikia kilele cha "utukufu utakaofunuliwa," ambao uta "funika ardhi kama maji yanavyoifunika bahari." Ni vigumu kimaandiko kukiri kuwa yeye ni Kristo, kwa upande mmoja, na kutojua ukweli huu mkuu wa Biblia, na kukataa baadaye uwazi ulioonyeshwa wa upakwamafuta wa Yesu, kwa upande mwingine.

Kristo kuwa mfalme wa baadaye wa ulimwengu ni mojawapo ya ukweli ya kuvutia wengi na wa furaha wa ufunuo wa Biblia. Ni matumaini yapi mengine yako pale kwa ajili ya dunia hii ya dhambi na taabu? Imeumia sana chini ya kongwa la utawala mbovu kwa miaka mingi. Utajiri wa dunia unaporwa na kundi dogo la wachache, na umati mkubwa wa binadamu unawachwa

kugalagala katika hali duni ya umaskini, ujinga, na taabu. Wema wa Mungu umepotea kwa udanganyifu.

Tutapata wapi faraja kwa siku za baadaye? Ulimwengu hautibiki kwa juhudi za binadamu. Matumaini yake ya pekee yamo tu katika ukweli kuwa Mkombozi mkuu anasubiri wakati uliowekwa wa baraka; Kristo aliye mkono wa kulia wa Mungu ni mfalme wa baadaye wa ulimwengu; yeye ambaye alistahimili aibu ya mtini kama mwenye kosa la jinai anakuja kuvaa heshima ya taji la uzima; na ingawa giza kuu litafunika mawingu ambayo yatakaribisha ujio wake mzuri, na degedege kali ambayo itahudhuria ukombozi wa dunia, jambo kubwa litakuwa tukufu siku atakapoleta, amani ya milele ambayo itakaa juu ya vilima vya milele.

MASWALI kwa somo la 24

1. Ni nini maana ya neno "Utawala wa kifalme wa Kristo"?

2. Wayahudi walitarajia nini kutoka kwa "Masihi" ?

3. Je, wafuasi walikuwa na matarajio gani kutoka kwa Kristo, Masihi?

4. Kama wanafunzi wake hawakuwa sahihi katika matarajio yao, ni nini baadhi ya matatizo makubwa sisi hukabiliwa nayo?

5. Ni usemi gani ulikuwa wa wazi wa manabii wa Agano La Kale kuhusu Utawala wa kifalme wa Masihi (Kristo)?

6. Wakati Biblia inasema "kiti cha enzi" cha Daudi, nini inaangaziwa kuhusu Daudi?

7. Kwa nini ni vigumu kwa Kristo kuketi katika kiti cha Daudi mbinguni?

8. Unabii uliosemwa na nabii Ezekiel uliashiria nini kuhusu ufalme wa Mungu kama ulivyokuwepo wakati huo?

9. Ni nani "Yeye" anayetajwa kwa matamshi ya unabii katika swali # 8 hapo juu?

10. Uhusiano wa Kristo na wafuasi wake wa kiroho ni upi?

11. Mfalme Herode alielewa kivipi tangazo la kuzaliwa kwa Yesu Kristo?

12. Maandiko yanatabiri nini kuhusu hali ya baadaye ya Yerusalemu?

13. Kwa nini Wayahudi walimsulibisha Kristo?

14. Neno "Kristo" ni neno la Kigiriki.

a) Ni nini usawa wake wa Kiingereza? b) Je, linarejelea nini?